

## HABARI ZA BIAS

# Latra yatangaza leseni kwa mabasi msimu wa sikukuu

Na Ikunda Erick

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza kutoa leseni za muda mfupi kwa wamiliki wa mabasi nchini ili kuongeza idadi ya magari yatakayohudumia abiria katika msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano wa Latra, Salum Pazzy akizungumzia hatua hiyo alisema leseni hizo zimeanza kutolewa Desemba 3, 2025 na zinatolewa kwa kuzingatia masharti na vigezo vilivyowekwa na mamlaka hiyo.

Miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na basi kuwa na uwezo wa kubeba abiria wasiopungua 40 au kuwa na leseni ya 'Special Hire', kuunganishwa kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), kuwa na bima iliyo hai.

Mengine ni kuwa na hati ya ukaguzi wa Polisi (VIR), kuwa leseni hai ya Latra na kuunganishwa kwenye mfumo wa Tiketi Mtandao.

Kwa upande wa madereva, Latra imesisitiza kuwa lazima wawe wamesajiliwa na kuthibitishwa na mamlaka hiyo, pamoja na kumiliki kitufe cha utambuzi kilichosajiliwa.

Pazzy alisema maombi yote ya leseni yatumwe kupitia mfumo wa leseni wa mamlaka na waombaji wanapaswa kuambatanisha nyaraka muhimu ikiwemo nakala ya kadi ya gari, bima, ukaguzi wa polisi na leseni ya udereva.

Mamlaka hiyo imesisitiza kuwa hatua hii inalenga kupunguza msongamano wa abiria na kuboresha huduma za usafiri katika kipindi chenye mahitaji makubwa ya usafiri.

Katika kuhakikisha abiria wanasafiri kwa wakati bila usumbufu, Latra kwa kushirikiana na wadau wa usafiri imeongeza usimamizi katika vituo vya mabasi kwa kuimarisha ukaguzi wa tiketi sambamba na kuratibu ratiba za safari za mabasi.

Aidha, mamlaka imewahamasisha watoa huduma kuongeza safari za ziada katika nyakati za msongamano mkubwa sambamba na kufuata vigezo na masharti yote ya leseni ili kuhakikisha usalama wa abiria, mali na chombo cha usafiri.

Aidha, mamlaka imetoa maelekezo kwa baadhi ya kampuni za usafiri kuongeza magari katika njia zinazokabiliwa na uhitaji mkubwa, huku ikiongeza doria na usimamizi ili kuhakikisha mabasi yanayoongezwa yanazingatia viwango vya usalama na sheria za usafiri.

Wakati huo huo imewahimiza wananchi kununua tiketi mapema kupitia mfumo wa Tiketi Mtandao ili kuepuka msongamano na ulanguzi wa nauli katika vituo vya mabasi, ambao mara nyingi hujitokeza kipindi cha sikukuu.

CamScanner

# Simulizi ndani ya basi la mwendokasi

Na REHEMA MAIGALA




MABASI Yaendayo Haraka maarufu 'mwendokasi', yamekuwa mkombozi kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wanaotumia usafiri huo kwenda katika maeneo mbalimbali kwa shughuli za uzalishaji mali.

Serikali ilibuni mpango huo kwa lengo la kupungumza changamoto ya usafiri wa mabasi hususani kwa wasafiri wanaokwenda maeneo ya katikati ya jiji Kariakoo na Posta.

Kabla ya kuanza huduma ya mabasi ya mwendokasi, ilishuhudiwa idadi kubwa ya watu vituoni kuanzia saa 10 alfajiri, ambapo msongamano huo ulikuwa kero kwa wafanyakazi, wafanyabiashara na wanafunzi waliokuwa wakitumia usafiri wa daladala kwenda katika shughuli za uzalishaji mali na shuleni.

Usafiri wa mabasi ya mwendokasi ni mfumo wa usafirishaji wa mabasi wa haraka ulioanza kufanya kazi Mei 10, 2016 jijini Dar es Salaam.

Mfumo wa usafirishaji una awamu sita na ujenzi wa awamu ya kwanza ulianza Aprili, 2012 na kampuni ya ujenzi ya Austria (Strabag International GmbH).

Ujenzi wa awamu ya kwanza ulikamilishwa Desemba, 2015 kwa gharama ya jumla ya Euro milioni 134 iliyofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania.

Awamu ya kwanza ya mradi ina urefu wa kilometa 21.1 katika barabara kuu tatu zenye vituo 29. Mfumo mzima unaendeshwa na Usafiri Salama Dar es Salaam (UDA-RT) chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Juu na Majini (Sumatra).

Mabasi yanatoa huduma kwa masaa 18 kila siku kutoka saa 5:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni na tangu kuanza kwake yamekuwa msaada mkubwa katika maeneo ambayo usafiri huo unatumika.

Itakumbukwa serikali ilianza kufanya mipango ya mfumo wa usafirishaji huo mwaka 2003 kutokana na ongezeko la watu zaidi ya milioni tano ifikapo mwaka 2015.

Usafiri huo na mfumo wa usafirishaji wa metro ulipendekezwa, lakini mfumo wa metro haukuidhinishwa kwa sababu ya gharama kubwa ya ujenzi na utendaji inayohusika.

Aidha, mradi uliwekwa chini ya ofisi ya Waziri Mkuu na Wakala wa Usafiri wa Haraka wa Dar (DART) uliundwa kupitia Ilani ya Serikali Mei 25, 2007.

Usafiri wa mwendokasi wa kilometa 130 ulipangwa kufikia zaidi ya asilimia 90 ya idadi ya watu wa jiji na mradi huo uligawanywa katika awamu sita kwa sababu ya uwekezaji mkubwa uliohitajika.

**MRADI WA MWENDOKASI**

Awamu ya kwanza ya mfumo wa BRT inaendesha kilometa 21 kutoka Kimara hadi Ubungo kuishia Kivukoni / Morocco. Ujenzi wa awamu ya kwanza ulianza Aprili, 2012 na njia yake imeundwa kubeba wasafiri 300,000 kila siku ikiwana vituo 29.

Njia hiyo ina kilometa 21 ya barabara kuu, kilometa 57.9 za barabara za kulisha, vituo vitano vikubwa na vituo 29.

Tangu kuanza usafiri huo, umekuwa mkombozi kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam ambao awali walikuwa wakikumbana na adha kubwa ya usafiri kutokana idadi kubwa ya watu vituoni.

Hata hivyo, usafiri huo uliingia dosari baada ya miundombinu yake kuharibiwa kwa kuchomwa katika maandano yaliyochochea vurugu yaliyofanyika katika uchaguzi mkuu Oktoba 29, mwaka huu, ambapo wakazi wa Mbagala ni miongoni mwa wananchi wa Dar es Salaam waliopata athari kubwa.

Hatua hiyo ilisababisha Serikali kutoa tamko la kusitisha huduma hiyo Novemba 5, mwaka huu ili kutoa fursa kwa wataalamu kurejesha miundombinu katika ubora wake kabla ya kuanza kazi hususani Mbagala.

Hivi sasa huduma ya usafiri kutoka Mbagala kwenda Posta na Gerezani imerejea baada ya kusitishwa kwa muda.

Kurejea kwa usafiri huo kumewaibua wananchi wanaotumia usafiri huo wakazi wa Mbagala ambao wanazungumzia faida na hasara ya usafiri huo, ambao kimsingi kwa upande wao umekuwa ni mkombozi.

Awali, baadhi wa wakazi wa Mbagala wanaofanya shughuli maeneo mbalimbali yakiwemo mjini Kariakoo na Posta, walikuwa wakiamka saa 10 alfajiri kuwahi usafiri wa daladala kwa lengo la kufika kwa wakati sehemu zao za kazi.

Pia, wanafunzi wa kada mbalimbali walikuwa wakiamka muda huo kuwahi usafiri wa daladala kwenda katika maeneo mbalimbali, lakini baada ya ujio wa mabasi ya mwendokasi wamepata ahueni kubwa.

Kabla ya ujio wa mabasi ya mwendokasi, vituoni asubuhi na jioni kulikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wakisubiri usafiri wa daladala, ambao hata hivyo walikuwa wakipanda kwa taabu huku wakitunishiana msuli na makondakta au madereva.

Ilikuwa ni kawaida kati ya wanafunzi 10 hadi 15 waliokuwa katika kituo kimoja cha daladala, wakapanda wawili au watatu, tena kwa masimango makubwa baada ya kuvimbiana na kondakta.

Baada ya ujio wa mabasi hayo, wananchi wa Mbagala wakiwemo wanafunzi wanafurahia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Wananchi hao wamesahau kadhia waliyokuwa wakiipata kwa muda mrefu kabla ya ujio wa mabasi hayo kama alivyosema mkazi wa Mbagala Kokoto, Abdulrahman Issa.

Issa alizungumza na mwandishi wa gazeti hili aliyekuwa miongoni mwa wasafiri wa basi hilo akitokea Mbagala kwenda Gerezeni, ambapo alifanya mahojiano na watu wa kada mbalimbali kuhusu ujio wa mwendokasi.

Issa alisema usafiri huo umekuwa mkombozi kwa wakazi wa Mbagala kwa sababu pamoja na idadi kubwa kusafiri wakiwa wamesimama, lakini hutumia muda mfupi kufika katika maeneo yao ya kazi au nyumbani.

Mwandishi wa makala haya alishuhudia utaratibu mzuri wa abiria kupanga foleni Gerezani kuingia ndani ya basi Gerezani, Kariakoo na Zakheim, Mbagala.

Issa alisema kumekuwa na utaratibu mzuri wa kupanda ndani ya basi Gerezani na Zakheim na hakuna 'vurugu' kama walivyokuwa wakitumia usafiri wa daladala vituoni.

"Ninaishukuru Serikali kwa usafiri huu umekuwa mkombozi kwetu, lakini wakati mwingine naona kama ndoto ingawa ni kweli, mabasi ya mwendokasi yamefika kwetu Mbagala

"Mimi ni mfanyabiashara, usafiri huu unanisaidia kwenda Kariakoo zaidi ya mara mbili awali nilikuwa siwezi kufanya hivyo si unaona hapa tumekutana nimekuja kuona bishara yangu, nyingine iko Mtaa wa Mafia na hivi sasa naelekea Mkuranga nikishatoka nakuja kufunga hesabu hapa Mafia,"alisema.

Hadija Issa, mzazi wa watoto wawili wanaosoma kidato cha kwanza na tatu katika Shule ya Sekondari Benjamini Mkapa iliyopo Kariakoo Dar es Salaam, alisema ujio wa mabasi hayo ni mkombozi kwa wakazi wa Mbagala.

"Kila siku ifikapo saa 12 jioni nilikuwa naanza kuwaza watoto wangu watarudi vipi kutoka shule, kwa sababu siku nyingine wanarudi saa tatu usiku hadi saa nne kwa sababu ya kukosa usafiri.

"Kuna wakati mwingine inanibidi nimtume bodaboda awafuate kwa kuwa mabasi ya daladala yalikuwa yakiwakataa wanafunzi,"alisema.

Hadija anashukuru Serikali kwa sababu usafiri wa mwendokasi umewarahisishia safari watoto wake hivi sasa wanarudi mapema nyumbani na wanawahi vizuri shuleni.

**KAULI YA MWANAFUNZI**

Mwanafunzi wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari Chang'ombe , Warda Ally, mkazi wa Mbagala Zakheim, alisema mabasi ya mwendokasi yamekuwa msaada mkubwa kwa kuwa wanawahi vipindi vya masomo.

Warda alisema kabla ya kuanza usafiri huo, mara kwa mara alikuwa akiadhibiwa shuleni kwa sababu ya kuchelewa vipindi vya darasani.

Alisema pia alikuwa akichelewa kufika nyumbani ambapo athari zake zilikuwa ni kubwa kwa kuwa alishindwa kufanya masomo ya ziada akiwa nyumbani.

"Naishukuru Serikali nilikuwa nikishindwa kufanya kazi zangu za shule vizuri kwa sababu ya uchovu wa kutembea umbali mrefu kutafuta usafiri

"Mimi nasoma Shule ya Changombe lakini daladla nilikuwa naifuata Mtongani, nilikuwa nachoka sana,"alisema ambaye alikuwa akiamka saa 10 alfajiri siku za masomo kujiandaa kwenda shule.

"Kuja kwa usafiri huu umenisaidia, nafika nyumbani saa 11 jioni ambapo awali nilikuwa nafika nyumbani kati ya saa 2.30 hadi saa tatu usiku,"alisema.

Dereva wa mwendokasi

Mabasi 27 ya mwendokasi yanayofanya safari zake Mbagala kwenda Gerezani, yamekuwa usafiri pendwa kwa wakazi wanaoishi maeneo hayo.

Mabasi hayo yanachukua muda wa dakika 35 kutoka Gerezani hadi Mbagala huku yakitumia dakika moja au moja kasoro kutoka kituo kimoja hadi kituo.

Akizungumza na gazeti hili dereva wa basi la mwendokasi Hamisi Shabani( si jina halisi) alisema abiria wa Mbagala wamefurahia kwa sababu hivi sasa wanafanya shughuli zao kwa uhuru na amani.

Hata hivyo, dereva huyo alisema hivi karibuni kutakuwa na mabasi yaendayo haraka ambayo kutoka Gerezani hadi Mbagala yatachukua dakika 12.

Alisema basi kubwa linabeba abiria hadi 150 ingawa uwezo wake ni abiria 70 wakiwa wamekaa katika viti wakati basi dogo linachukua abiria hadi 120 licha ya uwezo wake ni kubeba watu 53 wakiwa wamekaa.

Hata hivyo, dereva Shabani aliwaomba wananchi, magari madogo na bodaboda kuwa waangalifu wanapotumia barabara za mwendokasi kuepuka ajali.

"Mara nyingi ajali zinatokea na sisi madereva wa mwendokasi ndiyo tunalaumiwa, lakini wanaojiingiza katika miundombinu yetu siku zote wanakuwa si makini na kusababisha ajali ," alisema.

**MABASI YA MIZIGO**

Akizungumzia mabasi hayo, Shabani alisema UDART imetoa mabasi mawili ya kubeba mizigo ambayo hayo yanafanya safari zake Mbagala hadi Kivukoni.

Alisema mabasi hayo huanza safari zake saa 10 alfajili hadi saa nane mchana na kazi yao kubwa ni kubeba ndoo za samaki na mizigo mingine.

"Yapo mabasi mawili yametengwa kubeba ndoo za samaki na mizigo mingine, lakini ukimalizika muda huo yanaendelea kubeba abiria kama ilivyo kawaida," alisema Shabani.

**MCHUMI**

Kwa upande wake, mchumi Dk. Silvester Rugeihyam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema ujio wa mabasi hayo yatasaidia jamii kufanya kazi kwa wakati.

Alisema kuwahi kazini au sehemu ya uingizaji kipato kuna manufaa makubwa kwa sababu kutasaidia kupandisha kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa.

"Foleni imekuwa ni moja ya changamoto ya watu kutofanya vizuri katika shughuli zao, labda kwa mfano mzigo unahitajika ufike saa tatu asubuhi, lakini kwa sababu ya foleni unafika saa sita mchana hali hiyo inasababisha hasara kwa mfanyabiashara," alisema.

Dk. Rugeihyam alisema ubunifu wa mradi wa mwendo kasi ni moja ya chanzo cha maendeleo nchini, hivyo aliipongeza Serikali kwa hatua hiyo.

CamScanner